

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

S.L.P. 35091 ♦ DAR ES SALAAM ♦ TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

TANZIA



Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, anasikitika kutangaza kifo cha **Prof. Matthew Laban Luhanga (1948-2021)**, kilichotokea tarehe 16 Septemba 2021 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Marehemu **Prof. Luhanga** alikuwa Profesa katika Idara ya Uhandisi Elektronik na Mawasiliano pepe, Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (CoICT). Aliajiriwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa wadhifa wa Mhadhiri mwaka 1976. Alipandishwa vyeo vya kitaaluma hadi kufikia ngazi ya Profesa. Prof. Luhanga alistaafu rasmi utumishi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2018.

Prof. Luhanga alikuwa msomi na mwanataaluma mbobezi aliyetafiti, kuchapisha na kushauri katika maeneo ya "Telematics" hususani katika nadharia za kihisabati za mifumo ya mawasiliano (Mathematical Theories of Telecommunication Systems) na Elimu ya Uhandisi (Engineering Education). Prof. Luhanga alitoa zaidi ya machapisho 80 katika majarida yanayoheshimika duniani na vitabu 7. Aidha, alishiriki katika kazi mbalimbali za ushauri ndani na nje ya nchi. Vilevile alikuwa mwenyekiti/mjumbe katika kamati nyingi za kitaaluma na za ushauri.

Prof. Luhanga alishika nyadhifa mbalimbali ndani na nje ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikiwemo Makamu Mkuu wa Chuo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (1991-2006). Mojawapo ya kazi alizofanya katika Chuo Kikuu ni pamoja na kuanzisha na kusimamia Programu ya Mageuzi ya Kitaasisi (Institutional Transformation Programme-ITP). Aliwahi pia kushika nyadhifa nyingine zikiwemo Afisa Taaluma Mkuu (sasa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Taaluma) mwaka 1991; mwenyekiti na mjumbe wa bodi zaidi ya 70 zikiwemo TTCL, TCU, IUCEA, NECTA, NACTE, Tanzania Academy of Sciences, COSTECH, ITU-T, SUA, na MUHAS. Hadi kifo chake, Prof. Luhanga alikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu Mzumbe.

Mipango ya mazishi ya Prof. Luhanga inafanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na familia. Mwili wa marehemu unatarajia kuagwa Jumatatu tarehe 20 Septemba 2021 katika Ukumbi wa Nkrumah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mazishi yatafanyika siku ya Jumanne tarehe 21 Septemba 2021 katika Makaburi ya kwa Kondo, Tegeta.

Roho ya Marehemu Ipumzike kwa Amani!

**Imetolewa na Ofisi ya Uhusiano kwa Umma
17 Septemba, 2021**